

Swahili



Je, unahitaji mkalimani ili kufanya malalamiko kuhusu huduma yako ya ulemavu?

Tunaweza kupanga mkalimani kwa bure.

Tupigie simu kwenye nambari
1800 677 342

TTY: 1300 726 563
www.odsc.vic.gov.au



Ni sawa kulalamika



Disability
Services
Commissioner

Jinsi ya kufanya malalamiko kuhusu huduma yako ya usaidizi wa ulemavu.

Wakati mwingine watu hawana furaha kuhusu huduma yao ya msaada wa ulemavu.

Wewe unaweza kumwambia Kamishna wa Huduma za Ulemavu ikiwa unataka kuzungumza na mtu kuhusu huduma ya msaada wa ulemavu katika eneo la Victoria. Pia wewe unaweza kuuliza familia yako au marafiki wako kukusaidia kuzungumza na sisi.

Sisi tutafanya kazi na wewe pamoja na huduma ya msaada ili kufanya mambo vizuri. Huduma yetu ni bure kabisa na inajitegemea kutoka serikali na huduma zingine.

Watu wengine wanahitaji mkalimani ili waweze kutumia lugha isiyo ya Kiingereza wakati wa kuzungumza na sisi. Sisi tunaweza kukupangia mkalimani wa bure.

Ili kuzungumza na sisi:

- Tupigie simu kwenye nambari 1800 677 342.
- Tuambie nini kinachokufanya wewe usiwe na furaha.
- Tunaweza kuamua pamoja na wewe, nini cha kufanya baadaye.



OK



Ili kuipata brosha hii, tupige simu 1800 677 342.